**YAH: DIRISHA LA UDAHILI KWA AWAMU YA NNE - 2026/2027**

Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

2. Wizara ilipokea barua kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar yenye **Kumb No. AB.693/708/01/83** ya tarehe **21/08/2026** kuhusu ombi la kupatiwa fursa za mafunzo ya Ualimu, mchepuo wa Elimu Maalumu katika chuo cha Ualimu Patandi.

3. Ombi hili lilifanyiwa kazi na udahili ulifanyika kwa walimu kazini wanne (4) waliokidhi sifa na vigezo na kumi na mbili walikosa sifa za kujiunga. Aidha, ilielekezwa kufuata taratibu zote za udahili kwa wale wenye sifa ikiwemo kuomba nafasi ya mafunzo kupitia Mfumo wa TCMS.

4. Ili kutoa fursa ya mafunzo kwa wahitaji wa kundi hili, Dawati la udahili, Sehemu ya Ualimu itafungua mfumo wa TCMS kwa ajili ya dirisha la udahili awamu ya nne kwa mwaka wa masomo 2026/2027 kwa muda mfupi siku ya leo. Aidha, dirisha la usajili litafunguliwa ili kukamilisha taratibu husika.